# HADITHI YA IBRAHIMU (SEHEMU YA 6 KATI YA 7): SADAKA KUBWA ZAIDI

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Jaribio la maisha yote, Abrahamu anaona katika ndoto kwamba lazima amtoe sadaka “mwanae wa pekee”, lakini je, ni Isaka au Ishmaeli?

**Aina:** Makala Imani za Uislamu Hadithi za Mitume

**Na:** Imam Mufti

**Iliyochapishwa mnamo:** 10 Dec 2021
**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 18 Nov 2021

## Ibrahimu Amtoa Sadaka Mwanawe

Ilikuwa imekaribia miaka kumi tangu Ibrahimu kumwacha mke wake na mtoto huko Makka chini ya uangalizi wa Mungu. Baada ya safari ya miezi miwili, alishangaa kukuta Makka tofauti na jinsi alivyoiacha. Furaha ya kuungana tena ilikatizwa haraka na maono ambayo ingekuwa jaribu kuu la imani yake. Mungu alimwamuru Ibrahimu kupitia ndoto amtoe sadaka mwanawe, mwana ambaye alikuwa naye baada ya miaka mingi ya maombi na ndo alikuwa amekutana naye baada ya miaka kumi ya kutengana.

Tunajua kutoka katika Quran kwamba mtoto atakayetolewa sadaka alikuwa Ismaili, Mungu, wakati wa kutoa habari njema ya kuzaliwa kwa Isaka kwa Ibrahimu na Sara, pia alitoa habari njema ya mjukuu, Yakobo (Israeli):

***"…Basi tukambashiria (kuzaliwa) Is-haq, na baada ya Is-haq Yaaqub." (Quran 11:71)***

Vile vile, katika mstari wa Biblia Mwanzo 17:19, Ibrahimu aliahidiwa:

***"Sara mkeo atakuzalia mwana ambaye jina lake litakuwa Isaka. Nitalithibitisha agano langu naye kuwa agano la milele na uzao wake baada yake."***

Kwa sababu Mungu aliahidi kumpa Sara mtoto kutoka kwa Ibrahimu na wajukuu kutoka kwa mtoto huyo, kwa kimantiki wala kimatendo haiwezekani kwa Mungu kumwamuru Ibrahimu amtoe sadaka Isaka, kwa kuwa Mungu havunji ahadi yake, wala Yeye si "mwandishi wa kuchanganya."

Ingawa jina la Isaka linatajwa wazi wazi kuwa ndiye ambaye angetolewa sadaka katika Mwanzo 22:2, tunajifunza kutokana na muktadha mwingine wa Biblia kwamba ni tafsiri ya wazi, na aliyepaswa kuchinjwa alikuwa Ishmaeli.

# "Mwanao wa Pekee"

Katika mistari ya Mwanzo 22, Mungu anamwamuru Ibrahimu amtoe sadaka mwanawe wa pekee. Wanazuoni wote wa Uislamu, Uyahudi na Ukristo wanakubali, Ishmaeli alizaliwa kabla ya Isaka. Kutokana na hili, haingefaa kumwita Isaka mwana wa pekee wa Ibrahimu.

Ni kweli kwamba wasomi wa Kiyahudi-Mkristo mara nyingi hubishana kwamba kwa kuwa Ishmaeli alizaliwa na hawara, yeye si mwana halali. Hata hivyo, tayari tumeshataja hapo awali kwamba kwa mujibu wa Dini ya Kiyahudi, kuwapa waume zao mahawara kutoka kwa wake tasa ili wazae watoto lilikuwa jambo la kawaida, lililo halali na linalokubalika, na mtoto aliyezaliwa na hawara huyo angekua wa mke wa baba[1], kufurahia haki zote kama yeye, wa mke, mtoto wake mwenyewe, ikiwa ni pamoja na urithi. Zaidi ya hayo, wangepokea sehemu maradufu ya watoto wengine, hata kama "wangechukiwa"[2].

Zaidi ya hayo, imedokezwa katika Biblia kwamba Sara mwenyewe angemwona mtoto aliyezaliwa na Hajiri kuwa mrithi halali. Akijua kwamba Ibrahimu alikuwa ameahidiwa kwamba uzao wake ungeijaza nchi kati ya Mto Nile na Frati (Mwanzo 15:18) kutoka katika mwili wake mwenyewe (Mwanzo 15:4), alimtoa Hajiri kwa Ibrahimu ili awe njia ya kutimiza unabii huu. Alisema,

***“Tazama sasa, Bwana amenizuia kuzaa; nakusihi, uingie kwa mjakazi wangu; labda ninaweza kupate watoto kupitia kwake” (Mwanzo 16:2). (Mwanzo 16:2)***

Hii pia ni sawa na Lea na Raheli, wake za Yakobo mwana wa Isaka, kumpa Yakobo vijakazi wao ili wazae watoto (Mwanzo 30:3, 6. 7, 9-13). Watoto wao walikuwa Dani, Neftali, Gadi na Asheri, ambao walitoka kwa wana kumi na wawili wa Yakobo, baba wa makabila kumi na mawili ya Waisraeli, na kwa hivyo ni warithi halali[3].

Kutokana na hili, tunaelewa kwamba Sara aliamini kwamba mtoto aliyezaliwa na Hajari angekuwa utimilifu wa unabii aliopewa Ibrahimu, na kuwa kana kwamba alizaliwa kwa nafsi yake mwenyewe. Hivyo, kulingana na ukweli huu pekee, Ishmaeli si haramu, bali ni mrithi halali.

Mungu Mwenyewe anamchukulia Ishmaeli kama mrithi halali, kwa maana, katika sehemu nyingi, Biblia inataja kwamba Ishmaeli ni "uzao" wa Ibrahimu. Kwa mfano, katika Mwanzo 21:13:

***“Tena mwana wa mjakazi nitamfanya taifa, kwa maana yeye ni uzao wako.***

Kuna sababu nyingine nyingi zinazo thibitisha kwamba ni Ishmaeli na sio Isaka ambaye angetolewa sadaka, na mapenzi ya Mungu, makala tofauti zitawekwa kwa ajili ya suala hili.

Kwa kuendelea na simulizi hili, Ibrahimu alishauriana na mwanawe ili kuona kama alielewa kile alichoamriwa na Mungu,

***"Basi tukambashiria mwana aliye mpole. Basi alipo fika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini kuwa ninakuchinja. Basi angalia wewe, waonaje? Akasema: Ewe baba yangu! Tenda unavyo amrishwa, utanikuta mimi, Inshallah, katika wanao subiri." (Quran 37:101-102)***

Kwa hakika mtu akiambiwa na baba yake kwamba atauawa kwa sababu ya ndoto, haitachukuliwa kwa adabu njema. Mtu anaweza kutilia shaka ndoto hiyo pamoja na utimamu wa mtu huyo, lakini Ishmaeli alijua hali ya baba yake. Mtoto mchamungu wa baba mcha Mungu alijitolea kujisalimisha kwa Mungu. Ibrahimu akampeleka mwanawe mahali ambapo angetolewa sadaka na akamlaza kifudifudi. Kwa sababu hii, Mungu amewaeleza kwa maneno mazuri sana, akichora taswira ya kiini cha utii; ambayo huleta machozi kwa macho:

***"Basi wote wawili walipo jisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji." (Quran 37:103)***

Kisu cha Ibrahimu kilipokuwa karibu kushuka, sauti ilimzuia

***"Tulimwita: Ewe Ibrahim: Umekwisha itimiliza ndoto. Hakika hivi ndivyo tunavyo walipa wanao tenda mema. Hakika haya ni majaribio yaliyo dhaahiri." (Quran 37:104-106)***

Hakika ulikuwa mtihani mkubwa kuliko yote, kumtoa sadaka mtoto wake wa pekee, aliyemzaa baada ya kufikia uzee na miaka ya kutamani uzao. Hapa, Ibrahimu alionyesha nia yake ya kutoa sadaka mali yake yote kwa ajili ya Mungu, na kwa sababu hii, aliteuliwa kuwa kiongozi wa wanadamu wote, ambaye Mungu alimbariki na kizazi cha Manabii.

***"Na Mola wake Mlezi alipo mjaribu Ibrahim kwa kumpa amri fulani, naye akazitimiza, akamwambia: Hakika Mimi nitakufanya uwe mwongozi wa watu. Akasema: Je, na katika vizazi vyangu pia?" (Quran 2:124)***

Ishmaeli alikombolewa kwa kondoo dume,

***'…Basi tukamtolea fidia kwa dhabihu mtukufu.' (Quran 37:107)***

Ni mfano huu wa kunyenyekea na kumtegemea Mwenyezi Mungu ambao mamia ya mamilioni ya Waislamu huigiza kila mwaka katika siku za Hija, siku inayoitwa *Yawm-un-Nahr* – Siku ya Sadaka, au *Eid-ul-Adhaa* – au Sherehe ya Sadaka.

Ibrahimu alirudi Palestina, na baada ya kufanya hivyo, alitembelewa na malaika ambao walimpa yeye na Sara habari njema ya mwana, Isaka.

***"Wakasema: Usiogope. Sisi tunakubashiria kijana mwenye ujuzi." (Quran 15:53)***

Ni wakati huu ambapo pia anaambiwa kuhusu kuangamizwa kwa watu wa Lutu.

---

Rejeleo la maelezo:

[1] *Pilegesh*. Emil G. Hirsch na Schulim Ochser. Kitabu cha Kiyahudi. (http://www.jewishencyclopedia.com/view.jsp?artid=313&letter=P).

[2] Kumbukumbu ya Torati 21:15-17. Angalia pia: *Primogeniture*. Emil G. Hirsch na I. M. Casanowicz. Kitabu cha Kiyahudi. (http://www.jewishencyclopedia.com/view.jsp?artid=527&letter=P).

[3] *Jacob*. Emil G. Hirsch, M. Seligsohn, Solomon Schechter na Julius H. Greenstone. Kitabu cha Kiyahudi. (http://www.jewishencyclopedia.com/view.jsp?artid=19&letter=J).

Anwani ya wavuti ya makala hii:

https://www.islamreligion.com/sw/articles/298/hadithi-ya-ibrahimu-sehemu-ya-6-kati-ya-7

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2023 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.